



**WIZARA YA NISHATI
SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI
TANZANIA**



TAARIFA KWA UMMA

**UPOTOSHAJI WA UMMA KUHUSU TAARIFA ZINAHOHUSU MRADI WA BOMBA
LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (BOMBA LA EACOP)**

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) linapenda kuutaarifu umma kwamba, kufuatia kukamilika kwa makubaliano ya mikataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wawekezaji kuhusu Bomba la EACOP, wananchi wanashauriwa kuendelea kujisajili BURE kwenye Kanzi Data ya EWURA ili kupata fursa ya ujasiriamali katika Mradi.

Aidha, Serikali na Wawekezaji wamekubaliana kuwa fursa zote katika Mradi zitapatikana kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Serikali pamoja na makubaliano yaliyo fikiwa baina ya Serikali na Wawekezaji.

Hivi karibuni Serikali ilibaini kuwa kuna taasisi ya Jumuiya ya Watoa Huduma katika Sekta ya Mafuta na Gesi Tanzania (*Association of Tanzania Oil and Gas Service Providers [ATOGS]*) inaratibu na kuhamasiha ushirikishaji wa wajasiriamali katika Mradi kwa kulipa gharama, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu uliopo.

Serikali inasisitiza kuwa ATOGS haihusiki kwenye masuala yanayohusu Bomba la EACOP na haina mamlaka ya kuwezesha wajasiriamali kupata zabuni katika Mradi huo.

Wananchi wanahimizwa kuepuka matapeli kwa kujisajili kupitia Kanzi Data ya EWURA ili kupata fursa mbalimbali katika Mradi. Tunasisitiza kuwa taarifa rasmi za Bomba la EACOP kwa upande wa Serikali zitatolewa na Wizara ya Nishati kupitia taasisi zake za TPDC na EWURA au taasisi nyingine ya Serikali na si vinginevyo. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na *Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)* ili kusaidia wajasiriamali kushiriki katika Bomba la Mafuta la EACOP.

Kwa maelezo zaidi tembelea: www.tpdc.co.tz na www.ewura.go.tz

Imetolewa na:

Ofisi ya Uhusiano na Mawasiliano ya Umma (TPDC)